


# K.O.K.W.A

Na: Richard MWAMBE

©Jamvi la Simulizi 2025

## Ilipoishia...

**Kagera Bar Lounge, ndipo lile gari lilipokuwa limeegeshwa. Gina akatafuta mahala pazuri ambapo isingemsumbua kutoka kama ingehitajika kufanya hivyo kwa haraka. Wakabaki ndani kwanza.**

**"Tunafanyaje? Tunamvamia ndani au tunasubiri hapa mpaka atoke?" Gina akauliza.**

**"Gina, mbona una maswali sana leo vipi?" Amata akauliza.**

**"Nna hamu ya kazi…"**

**"Sawa, nenda ndani ya hiyo bar hakikisha unamnasa, nakupa nusu saa tu…" Amata akamwambia.**

**"Sasa nitamjuaje?" Gina akahoji kwa utulivu.**

**"Nenda, mwambia DJ atangaze kuwa mwenye gari aina ya Mazda Jeusi mtajie na namba anahitajika nje, atatoka utamuona!" Amata akatoa maelekezo.**

## SEHEMU YA 07

"Kazi ndogo sana!" Gina akajibu na kutoka kwenye lile gari huku akimwacha Amata. Hatua zake za kike zilimfikisha kwenye mlango wa kuingia kwenye klabu ile. Kamanda Amata alikuwa akimtazama mwanamke huyo katika kila hatua. Dakika tano

zilipita, Amata hakuona chochote kinachoendelea. Dakika kama ya nane hivi, Amata akamwona Gina akitoka nje na kusimama kando ya lile gari. Halafu muda mdogo baadae kijana mmoja alitoka kwenye ule ukumbi na kuliendea lile gari. Mazungumzo ya dakika kama tatu hivi yalifuata katika ya Gina na yule kijana kisha woye wawili wakaingia ndani. Simu ya Amata ilitetemeka. Arafa moja iliingia. Akainyakua na kuparaza kioo chake. Kulikuwa na ujumbe kutoka kwa Gina. Akaufungua.

*'Amekolea, natoka naye si muda'*

Baada ya kuisoma, akafunga simu yake na kuirudisha pahala pake. Kutoka katika kiti chake akahamia kiti cha dereva na kukaa nyuma ya usukani. Akavuta droo ya gari lile na kutoa bastola iliyokuwamo. Akaifyatua magazine na kuangalia kilichomo. Akatikisa kichwa juu chini ikiwa ni ishara ya kuridhika na alichokiona. Amata alikuwa akisinzia, lakini alijitahidi kutumia nguvu nyingi kupambana na usingizi huo. Ilimchukua dakika kumi na tano kushtushwa kwa kumwona Gina akitoka ndani ya ile klabu akiwa kakumbatiwa na yule jamaa. Ingawa moyo ulimuuma Amata lakini ilimpasa kuvumilia kwani kila kilichofanyika ni kwa ajili ya kazi. Yule mwanaume akamwingiza Gina kwenye lile Mazda kisha yeye akazunguka upande pili na kukaa nyuma ya usukani. Dakika moja baadae lile gari likaondoka pahala pale. Kamanda Amata akawasha gari lake na taratibu kuliondoa katika maegesho na kulifuata windo lake. Alipokaribia barabara kuu, aliliona lile gari likikunja kuhoto na kuchukua uelekeo wa Manzese. Naye akaunga tela na kuwafuata. Kati yake na lile gari akayaruhusu mengine matatu ili kumpoteza bwana

yule kujua kuwa anafuatiliwa. Lile gari liliiacha Barabara ya Morogoro na kukunja kulia kuelekea Shekilango. Amata naye akakunja hukohuko na kuendelea kulifuata. Katika Barabara ile mara tu baada ya kupita Sinza Makaburini, lile gari lilikunja kulia na kufuata uelekeo wa Hoteli ya Rungwe. Lile gari liliegeshwa nje ya hoteli hiyo. Amata akaingia gari lake kwenye bar ya jirani ambayo kwayo ulevi ulikuwa ukiendelea. Akapachika bastola yake kiunoni na kuifunika kwa shati lake alilovaa. Akatoka na kufunga mlango vizuri. Kwanza akaifuata kaunta ya ile baa na kuagiza bia ya Kilimanjaro baridi. Akapiga mafunda matatu tu ikamaliziaka. Hii yote ilikuwa ni kuwapa muda wawe tayari chumbani. Labda walau jamaa atapata hata denda la mwisho katika uhuru wake wa uraiani maana kuna mawili; ama afe usiku huu au aende lupango. Dakika tano zilikatika. Amata akalipa na kuondoka kwenye ile baa kuielekea ile hoteli. Simu yake ikatetemeka, akaichukua na kuifungua.

*'Room number 35'*

Hiki ndicho alikuwa akikisubiri haswa. Aliufikia mlango mkubwa wa hoteli ile, akaicha mapokezi kulia yeye akazielekea ngazi. Kwa hatua za haraka haraka, akapanda vidato vya ngazi mpaka sakafu ya tatu. Pale akapokelewa na korido ndefgu iliyotandikwa zuria jekundu. Akazivuta hatua ndefundefu mpaka mlango namba tano. Akasimama mbele yake. Akaipapasa bastola yake, ipo. Hakuichomoa. Kutoka ndani alisikia sauti ya Gina akiwa katika ubishani na mwanaume huyo. Hakujali kusikiliza wanachobishania lakini akilini mwake kama mwanaume

alishajua. Akagonga hodi na kusubiri akiwa tayari kwa dhoruba yoyote. Yale mabishano yakakoma. Akagonga tena na kusubiri.

"Nani?" akasikia sauti nzito ya kiume kutoka ndani.

"Fungua! Mi Braison…" Amata akajitambulisha kwa jina la rafiki wa mwanaume huyo ambaye mpaka wakati huo wala hakuwa tayari kamjua jina lake. Funguo ikazungushwa kutoka ndani. Kitasa kikanyongwa, mlango ukafunguliwa. Amata akabaki kasimama katikati ya mlango akitazamana na mwanaume yule aliyekuwa kifua wazi.

"We ni nani?" yule mwanaume akauliza. Kabla hata hajajibiwa, alijikuta akipokea pigo zito la karate lililotua sawia kwenye paji la uso. Yule mwanaume akaenda chini mzima mzima. Amata akaingia mule chumbani na kurudishia mlango nyuma yake. Tayari damu zilikuwa zikimvuja puani kwa fujo. Alijaribu kujiinua lakini alishindwa. Amata akapachika mkono wake kwenye mkanda wa suruali yake na kuchomoa kisu kidogo.

"No-no-no…" yule jamaa alilalama kwa maumivu lakini hakuwa anataka kusubiri kile ambacho Amata alinuia kufanya.

"Unaikumbuka ajali ya majuzi pale Mtaa wa Samora?" Amata akamuuliza na yule bwana akajibu kwa kutikisa kichwa.

"Kwanini mlitaka kumuua yule mama?"

"Ooooh mi-mi mimi nilipewa maagizo tu!" yule jamaa akajibu.

"Nani alikupa maagizo?"

"Boss… ni boss a-a-alinipa maagizo… usi-ni-niue tafadhali, nitakupa ushirikiano," yule jamaa akajibu akitetemeka. Gina alikuwa pembeni kimya.

"Bosi wako ni nani?" Amata akahoji.

“Braison Sambala…” akajibu huku akijiinua. Amata akaingiwa na huruma, aliona wazi huyo jamaa hana lolote la kumzuru, alikuwa kibaraka mdogo tu asiyejua hata mapigano.

“Usiinuke, damu zitatoka zaidi… lala hivyo hivyo!” akamwambia kwa upole. Gina aliyekuwa pembeni akapigwa na butwaa kuona huruma ya Amata. “Braison Sambala yupo wapi?” Amata akauliza.

“Yupo Kunduchi Beach Resort!”

“Chumba namba ngapi?” Amata akataka kujua.

“Kumi na saba mzee…”

“Good, sasa nataka umpigie simu, umwambie kuwa unahitaji kuonana naye, mimi nina shida na Braison siyo wewe…” Amata akamwambia huku akichukua simu kitandani na kumkabidhi yule jamaa. Akaichukua kwa mikono ya kutetemeka na kubofya namba kadhaa kisha akaiweka sikioni. “Weka loud speaker!” Amata akamwambia.

“Comrade!” yule jamaa akaita kwa sauti ya upole.

“Vipi wewe? Mbona unapiga simu nje ya muda?” mtu wa upande wa pili akauliza. Amata akagundua haraka kuwa watu hao wana mida maalumu ya kuligiana simu. Hiyo ni ,oja ya mbinu za majambazi kama hawa.

“Tuonane! Dharula!” akamwambia maneno hayo mawili tu.

“Njoo Kunduchi,” mtu wa upande wa pili akajibu. Amata akaichukua ile simu na kuikata. Akaitia mfukoni.

“Vaa shati tuondoke… sisi hatukuhitaji wewe tunamtaka Braison,” Amata akamwambia huyo jamaa. Alipomaliza kuvaa shati, pingu ikapachikwa mikononi pake. Safari ya kutoka Hoteli ya Rungwe kuelekea Kunduchi ilianza. Tayari usiku ukikuwa

ukiyoyoma wakati Amata na Gina walipokuwa kwenye msako mkali.

✠ ✠ ✠

## Kunduchi Mtongani Beach Resort

Inspekta Simbeye na timu yake tayari walikishawasili katika resort ile. Waligawana maeneo na kila mmoja alikuwa akiendelea na burudani yake wakisubiri bosi wao atawaamuru nini. Hata yeye Simbeye alikuwa hapo lakini hakujua ni nini hasa Amata alichomuitia hapo na kumtaka afike na kikosi chake. Kikosi kinachoogopwa kama corona Dar es salaam yote kwa operesheni yao dhidi ya ujambazi. Kila mmoja alikuwa na silaha ndogo aliyoificha vizuri. Hapa walisogea na gari binafsi, Toyota Mark II. Walikuwa watatu. Halafu watatu wengine walikuja na Defender lakini walilificha sehemu kisha wao wakaja kwa mguu. Simbeye alikuwa kaunta kabisa, hata ungemwona, husingemjua kwani jinsi alivyovalia alikuwa kama 'pedejhiee' fulani.

Amata, Gina na yule jamaa walitumia dakika arobaini na tano kufika pale. Gina aliendesha gari taratibu kabisa kutafuta maegesho. Alipopata, akaliegesha lile gari.amata akamtazama yule jamaa kwa jicho ambalo halikuwa na masihara hata kidogo, "Nakufungua pingu, utanitangulia hatua ishirini kwenda alipo Braison, sawa, usilete uhuni maana hii resort yote sasa hivi imezungukwa na askari," akamwambia huku mkononi tayari alikuwa na funguo ya kufungulia ile pingu.yule bwana akajibu kwa kutikisa kichwa huku kijsaho chembamba kikimtiririka. Mlango ukafunguliwa, akateremka. Alipovuta hatua kama kumi hivi, Amata naye akateremka na kumfuata kwa nyuma. Tayari

alikwishawashtua Simbeye na vijana wake kuwa amefika wakae tayari, akawaambia na eneo gani analoelekea. Wale vijana wakajipanga haraka kwa namna ya ajabu. Lakini bado walikuwa kama watu wasiyofahamiana. Amata akamwacha yule bwana apande ngazi za mbele, yeye haraka akawahi ngazi za nyuma. Kisha wakakutana kwenye korido. Kamanda Amata jakuonesha kama yupo na huyo bwana, yeye alikuwa akipita tu kwenye ile korido wakati yule bwana akigonga mlango wa Braison.

✠ ✠ ✠

Ndani ya chumba kile alikuwamo Braison Sambala na mwanamke mmoja aliyempata hapohapo resort. Mwanamke aliyezielewa pesa za kijana huyo bila kumjua yu nani. Hilo siyo swala lake, yeye alikuwa akitaka 'pochi'. Hodi iliyobishwa ilitambuliwa na Braison, maana huo ulikuwa mtindo wao wa kugongeana milango. Akakiacha kitanda na yule mwanamke, akauendea mlango akiwa na taulo tu. Hakujiuliza wala hakuchezwa na machale, alinyonga funguo na kuvuta kitasa, mlango ukafunguka. Ni kweli kwamba alimwona rafiki yake aliyempigia simu, lakini kabla hata hajamkaribisha ndani alijikuta akipokea pigo moja matata sana lililompepesua na kumbwaga kando. Chupa za pombe zilizokuwa mezani zikatawanyika na kuvunjika. Yule mwanamke akatoka kitandani na kurukia kwenye kona huku akijifunika na shuka aliyowahi kuivuta maana alikuwa uchi. Braison aliinuka haraka na pande la chupa mkononi, akarusha mkono wake kumuelekea Amata huku ameuma meno, Amata akaruka nyuma, na ile chupa ikamkosakosa na kuchana shati. Akabonyea chini na kuachia konde zito lililotua sawia tumboni. Akambeba Braison na

kumsukuma mpaka ukutani puuu! Akamwachia kisha akamchapa makonde matano ya kilpo nyingi yaliyoangusha meno mawili. Braison alikuwa chini hoi, mwili wake ukitawanyika huku na huko. Amata akafunga saa yake vizuri. Braison alikuwa akitweta kama jibwa lililokimbizwa.

"We! Vaa nguo zako uwende!" Amata akamwambia yule mwanamke aliyekuwa na Braison. Kwani hata alikumbuka kuvaa kwenyewe? Alizikusanya na akabeba na mkoba wake akatoka hivyohivyo. Alivalia wapi, sijui. "Aliyekwambia utaikimbia Jamhuri nani?" Amata akauliza. Inspekta Simbeye, naye akawasili na vijana watatu katika chumba kile.

"Weldone Amata!" Simbeye akampongeza Amata huku akivua kofia yake kubwa aliyoivaa muda wote.

"Mzee, chuku mtu wenu huyu, nitamkuta ofini kwako usiku wa leo hiihii ana maswali ya kujibu, naomba awe katika hali nzuri ya kunijibu…" Amata akasema. Wale vijana wakaingia ndani na kumkamata Braison, wakamuinua na kumtia pingu. Wakachukua suruali wake na kumvalisha, juu hawakujali. Wakamvika fuko jeusi kichwani na kutoka naye mzobe mzobe.

"Asante sana, huyu mshenzi ametukimbia kwa miaka mingi sana!" Simbeye akajibu huku akiondoka eneo lile. Hapo ndipo Amata alipogundua kuwa yule bwana aliyemleta hapo hayupo. *Doh! Hakuwa wakuachiwa yule mshenzi, naye ana ya kujibu!* Akawaza. Lakini hakuona haja ya kufuatilia. Akafunga ule mlango na kuanza kukikagua kile chumba. Simu mbili za Braison akazichukua, kadi za benki na kadi kazi za watu mbalimbali nazo akazibeba. Chini ya mto wa kitanda akakuta bastola kubwa ya revolver ikiwa full kwenye magazine yake. Akaichukua na kuitia kwenye kifuko cha plasitiki. Akatazama vizuri kila kona, hakuna

kingine. Akatoka kwenye chumba kile akiwa na begi la Braison na mkoba mwingine alioweka vile vitu. Akatumia ngazi za nyuma kuteremka mpaka upande wa baharini. Akavuta hatua na kupita upande mwingine mpaka kwenye maegesho. Akaingia garini na kuketi. Gina hakuwapo. Akapiga honi katika mtindo wao wa kuitana, kisha akasubiri. Dakika moja tu, Gina aliingia na kuketi nyuma ya usukani.

"Yule mshenzi kanichomoka wakati napambana na Braison!" Amata akasema.

"Hajakimbia, niliwapa taarifa vijana wa Simbeye wamemdakia hapo ng'ambo ya barabara karibu na Mama Joy Saloon, wameondoka naye…" Gina akaeleza huku akiwasha gari. "Tunaelekea wapi?"

"Catral Police kwa Simbeye, nataka nikamhoji yule mshenzi," Amata akajibu. Gina akaingiza gari barabarani na kupotea zake. Ilikuwa tayari inakaribia saa sita usiku wakati Gina akiwasili eneo la Mwenge. Amata alikuwa akisinzia na kushtuka wakati wote.

"Umechoka sana mpenzi!" Gina akaongea na kuiacha Barabara ya Bagamoyo, akatoa gari pembeni na kusimama karibu na eneo la ITV.

"Vipi?" Amata akauliza.

"Unaonaje ukipumzika kwanza halafu kesho ndiyo umuhoji huyo mshenzi?" Gina akatoa pendekezo kutokana na uchovu aliouaona wazi kwa Amata, "maana tangu umefika kutoka safari, hujalala kabisa," akamalizia.

"Gina, nitapumzika… kuna eneo nataka kufika katika hili jambo kisha nitahitaji kupumzika na nitakuhitaji wewe

kunipumzisha," Amata akajibu na kuachia tabasamu pana. Tabasamu la bei mbaya.

"Lini Amata, nakuju wewe, nakujua vizuri… kumbuka afya yako ndiyo mtaji wako," Gina akabembeleza.

"Ni kweli… nahitaji kumhoji Braison nikimalizana naye nitapanga kupumzika hata kama ni kesho. Ila yule mshenzi ni wa kuhoji usiku huu," Amata akasema. Gina akaingiza gara barabarani na safari ikaendelea. Kamanda Amata, akaitoa simu ya Braison na kujaribu kuifungua, ikagoma. Ilikuwa imefungwa kwa pateni ngumu. Akachukua ya kwake na kuskani padi ya namba ya simu ile ya Braison. Kutokana na mfumo wa utambuzi uliofungwa kwenye simu ile ya Amata, ikamwonesha mchoro wa pateni unaochorwa mara nyingi katika simu ile. Akajaribu kuurudia, ikafunguka. Akafungua kikasha cha mawasiliano, hakukuta jina hata moja. Alilitegemea hili. Majambazi wengi hupende kuhifadhi majina muhimu kichwani na si kwenye simu zao. Akarudi kwenye kikasha cha ujumbe mfupi. Hapa napo hapakuwa na ujumbe wowote ule, kikasha kilikuwa tupu kabisa. Amata akashusha pumzi ndefu.

"Vipi?" Gina akauliza.

"Mshenzi huyu hajahifadhi kumbukumbu yoyote kwenye simu yake," akamjibu huku akiendelea kupekua ile simu. Aliporudi kwenye simu zilizopigwa, ndipo akakutana na namba nne tu zilizopigwa siku hiyo. Mojawapo ya namba hizo ilikuwa ile ya yule swahiba wake. Aliitambua kwa kuangalia muda ambao simu ile ilipigwa. Namba tatu za mwisho, akazihifadhi kwenye kijitabu chake kisha akainakili na namba ya simu ile. Akahifadhi zote kwenye simu yake. *Zinahitaji kufanyiwa ukaguzi wa haraka!* Akajisemea moyoni.

Gina akaegesha gari nje ya jengo la Polisi kituo kikuu katika Barabara ya Railway. Alipozima injini tayari Amata alikuwa akikwea ngazi kuelekea kaunta ya kituo hicho. Utulivu natika kituo hicho ulikuwa mkubwa sana, unaweza kufikiri umefika kanisani kumbe la.

"Naweza kumuona Inspekta Simbeye?" akauliza.

"Bila shaka, karibu upande huu," konstebo aliyekuwa mezani hapo akamuongoza Amata mpaka ofisi nyingine na si ile aliyoizoea. Ofisi ile katika muimo wa juu wa mlango palibandikwa kibandiko kilichosomeka 'Upelelezi Mkoa'. Humo alikuwamo, Inspekta Simbeye na wanaume wengine wanne. Kati yao ni mmoja tu alikuwa kavalia sare za kipolisi na mabegani pake zilionekana nyota mbili ziking'aang'aa.

"Karibu sana," Simbeye akamkaribisha Amata na kupewa kiti. "Huyu ni mgeni wetu, labda hamjawahi kukutana naye, ni ASP Jaffari, kazi maalum. Baada ya kumtambulisha, salamu za kijeshi zikafuata, kwani aliyeingia hapo alikuwa Mrakibu Msaidizi wa Polisi. Pasi wao kujua kuwa cheo hicho ni utambulisho bandia salamu za utii zilitolewa, naye akazipokea.

"Asante, nimekaribia…"

"Ndiyo umekuja kwa ile kazi?" Simbeye akauliza.

"Naam… na nina dakika thelathini tu niwe nimeimaliza…" Amata akajibu. Simbeye akainuka na kufuatwa na wale vijana wawili. Pale wakamuacha yule mwenye sare za polisi na nyota zake mbili.

Katika chumba chenye ukubwa wa wastani, Amata aliingia na Simbeye pamoja na wale askari wawili waliokuwa wamevalia kiraia. Katikati ya chumba kile, palikuwa na meza ya chuma na viti viwili; upande huu na upande ule mwingine.

“Nileteeni ndoo ya maji!” Amata akaomba, na ombi lake likatekelezwa. Braison Sambala aliingizwa kwenye kile chumba kwa kusukumwa. Alikuwa hataki kuingia na alikuwa mbishi. Katika purukushani zile, askari mmoja alianguka na kuumia vibaya. Amata aliwaamuru wamuache na wamfungue pingu. Kila askari alihofu kutokana na ukorofi wa Braison. Macho mabaya ya jambazi huyo yalikuwa kwa Amata huku akitweta kwa nguvu. Amata akaomba funguo ya ile pingu na kupatiwa. Kila mmoja alikuwa akiangali nini kitatokea. Akamfikia na kumguza nyuma kisha akapachika ile funguo na kufungu ile pingu. Ilipoachia upande mmoja, Braison alitumia mkono ule kumpelekea pigo la kichwani. Kama isingekuwa wepesi wa Amata pingu ile ingempasua vibaya kichwani. Lakini Amata alishajua kuwa mwanaume huyo anaweza fanya lolote hapo maana hana la kupoteza. Amata aliepa, ile pingu ikapita kwa kasi jirani ya sikio lake. Mvumo wake wa kuogofya ulizifikia ngoma za masikio yake. Aligeuka haraka na pigo moja lililotua kwenye uti wa mgongo wa Braison. Kabla hajakaa sawa, alipokea mtama mmoja wa kilo nyingi na kabla hajatua chini aliinuliwa na pigo jingine la teke lililomtupa akatua nusu sakafuni nusu mezani. Akaanguka vibaya na kutoa yowe la maumivu. Amata akatulia wima sakafuni.

“Bado unataka kupigana?” Amata akamuuliza huku yule jamaa akijizoazoa kuinuka. Akamkamata vizuri na kumkalisha kitini kwa nguvu.

“Nani amemuua Kisinini?” Amata alimuuliza huku akimfunga mikono yake kwenye vyuma vya ile meza.

“Sijui! Usiniulize maswali ya kise***” Braison akajibu kijeuri huku damu zikimvuja puani.

“Majeuri ndiyo daima huwapenda kwenye kazi yangu,” Amata akasema na kuchukua mkasi wa kukatia nguo. Akasimama nyuma ya Braison, “Nitakukata masikio yote, na sintojali hata kama utakufa, sina undugu na wewe…” akamwambia na kumkamata kichwa sawasawa, mkasi ukalishika sikio na Amata akaanza kuvikutanisha. Mkasi ulianza kula nyama za lile sikio huku likikatika taratibu. “Nani kamuua Kisinini?” Amata akaendelea kuuliza huku akiendelea kukata lile sikio. Braison alipiga kelele za uchungu na kuuma meno. Akajaribu kujitikisa lakini mikono yake ilikuwa imefungwa barabara kwenye ile meza ya chuma. “Usipojibu namaliza sikio hili naanza jingine,” Amata alimwambia Braison huku akiendelea kukata lile sikio. Matuai mazito yalikuwa yakimtoka jamabazi huyo lakini kwa Amata ilikuwa kama wimbo mzuri masikioni pake. Sikio la kulia la Braison lilikuwa mezani. Damu zilimmwagika bila mpangilio. Braisona alilia kama mtoto.

“Usiponipa jibu, tunaanza sikio jingine,” Amata akamwambia huku akiketi kwenye kiti kilicho mbele yake. Wakatazamana. Utaniambia au hutoniambia? Nina maswali matatu tu, nani kamuua Kisinini? Kifo cha Kisinini kina uhusiano gani na upotevu wa Kokwa na kwanini mlifanya ajali ya kumuua mama yangu?” Amata almuorodheshea maswali kisha akainuka na kuelekea upande wa pili tayari kuanza kukata sikio jingine.

“Noooooooo!” Braison alipiga kelele. Inspekta Simbeye akatoka kwenye kile chumba na kuwaacha wale askari wengine wakitazama mateso hayo ambayo hata wao huwa hawayafanyi kwa mtindo huo.

“Afande niletee na yule mwingine!” Amata akaomba yule kijana mwingine aliyekuwa akiendesha lile Mazda afikishwe

kwenye kile chumba. Dakika moja tu iliyofuata akaingizwa mule ndani akiwa kafungwa pingu. Yule bwana alikuwa akitetemeka baada ya kuziona damu zilizotapakaa pale mezani na sakafuni. “Braison, haya nijibu swali langu moja baada ya jingine,” Amata akamwambia na kukimata kichwa cha jambazi yule kwa nguvu na mkasi ukaka vyema katika sikio lake. Yule bwana aliyeletwa akajiziba macho kwa mikono yake yenye pingu. Ile mikono ikashushwa kwa nguvu.

“Unatakiwa kutazama!” askari mmoja akamwambia.

“Haya nijibu swali la kwanza…” Amata akamwambia Braison na kuanza zoezi lake la kukata lile sikio.

“Aaaaaaiiigh! Shetan mkubwa wewe…” Braison akalia kwa uchungu.

“JIbu swali…” Amata akamwambia.

“Niue tuuuu, sintokwambia lolote!” Braison akajibu kijeuri. Amata akaongeza kuminya vidole, ule mkasi ukazidi kukata nyama ya sikio.

“Wewe!” Amata akamwita yule jamaa aliyeletwa mule ndani, “Jiandae kujibu maswali yangu!” akamwambia. Yule bwana tayari alikuwa amekwishajikojolea muda mrefu, nguvu ilikuwa ikimwishia taratibu. Amata alimkazia macho. “Khhhaaaaaa! Umejikojolea?” akamuuliza. Amata akaondoa mkasi kwenye sikio la Braison, akawatazama wale askari wawili waliokuwa pale, “Afande, niitie daktari wa polisi, mwambie aje na vifaa vya kushona jeraha la binadamu, aje sasa hivi kabla sijaondoka,” akampa maagizo. Akaweka mkasi mezani na kumtazama yule kijana. “Natala uniambie, nani aliyemuua Kisinini asubuhi ya jana?” akamuuliza.

“Ki-ki-ki-kisinini?”

"Ndiyo!"

"Br-Bra-Braissson!" akajibu huku akitetemeka kwa uwoga.

Amata akamtazama Braison, "Kumbe wewe ndiye umemuua Kisinini… sasa nataka ukiambie nani alikutuma, nyang'au wewe…" Amata alishikwa na hasira.

"Mwacheni jamani nitawajibu mimi…" yule jamaa mwingine akajibu. Macho yake yalikuwa yakimbubujika machozi. Huruma! Amata akamtazama.

"Unamjua nani aliyemtuma huyu kumuua KIsinini?" Amata akamuuliza yule bwana.

"Ndiyo, ni tajiri mmoja mzungu namjua kwa jina moja tu… Maiko," yule bwana akajibu.

"Na aliyewatuma mfanye ajali ya kumuua yule mama ni nani?" Amata akauliza kwa ukali.

"Ni huyohuyo Maiko…" akajibu.

"Umesema Maiko ni mzungu?"

"Ndiyo!"

"Anaishi wapi?"

"Yeye amefikia hotelini tu… tulienda kukutana naye siku nne zilizopita, akatupa kazi nne za kufanya…" yule bwana akabwabwaja. *Huyu siyo mzoefu wa kzi walikuwa wakimfanya nchambo tu!* Amata akawaza. "Enhe nitajie hizo kazi…" Amata akamwambia yule bwana.

"Tuliambiwa tumuue Selina, huyu tuliambiwa ni mwanamke hatari sana hapa Tanzania…" akaeleza. Amata akashtuka kusikia hivyo. Selina ni Madam S. "Pia tulitakiwa kumuua Kamanda Amata!" akaendelea kusema. Amata alihisi kuingiwa na ubaridi kuanzia utosini mpaka unyayoni.

"Enhe!" akamtaka kuendelea.

“Pia tulitakiwa kumuua Geophrey Kisinini na Tabia Ismail,” yule bwana akaeleza pasi na kumumunya maneno. Kamanda Amata akajikuta anaishiwa nguvu. Akameza mate na kuitazama saa yake. Ilikuwa ikiyoyoma kuelekea saa tisa usiku. “Maiko mlikutana naye wapi hapa Dar es salaam?” akauliza.

“Tulikutana naye nyumbani kwake Kibada…” akajibu.

“Kibada? Ok! Nikikwambia unipeleke unaweza?” Amata akauliza. Yule bwana akajibu kwa kutikisa kichwa kwamba ‘ndiyo’. Wakati akihojiana na bwana huyo, tayari daktari alikuwa amewasili na kazi ya kushona masikio ya Braison ilianza. Amata akatoka kwenye kile chumba na kurudi katika ofisi ile ya upelelezi Mkoa. Pale akamkuta Inspekta Simbeye peke yake.

“We mshenzi siyo binadamu hata kidogo…” Simbeye akasema.

“Tukiwa kazini hatuna mzaha hata kidogo. Asante mzee mi nimemaliza, sasa huyo ni wa kwenu siyo wangu tena. Mimi niachieni yule mwingine bado sijamalizana naye,” Amata akamwambia, “tuonane kesho, nitalutafuta,” akamwambia huku akipotelea nje. Kamanda Amata akamchukua askari wa mapokezi na kumkabidhi vifaa vyote vya Braison Sambala kisha yeye akaingia garini. Gina alikuwa amelala fofofo nyuma ya usukani.

“We msichana, amka twende…” akamwambia Gina huku akimtikisa. Gina akakurupuka na kujiweka vizuri. Akajifikicha macho.

“Uuuuh nimechoka sana… tunaelekea wapi, saa tisa sasa…” Gina akauliza.

“Twende nyumbani kwako sasa tukalale…” Amata akamjibu. Gina akatabasamu na kuwasha gari.

“Hayo ndiyo maneno dear… nimemiss sana joto lako…”

“Endesha gari!”


**Wasiliana name kwa Whatsapp**

**0766974865**